



duduaceho.com

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo unahamasisha utegemezi wa wakulima wadogo

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo unahamasisha matumizi makubwa ya mbegu chotara na mbolea za chumvichumvi na matokeo yake ni kuwa na utegemezi mkubwa wa wakulima na matatizo ya kifedha kwa nchi kadhaa Kusini mwa Afrika:

- ▶ Nchini **Botswana**, ISPAAD haijawahamisha wakulima kuelekea kwenye uzalishaji wa kibiashara, badala yake, kwa kiasi kikubwa imeongeza idadi ya wakulima wa kujikimu.
- ▶ Nchini **Lesotho**, mpango wa pembejeo za kilimo umewafanya wakulima kutegemea usambazaji wa pembejeo za bure daima.
- ▶ Nchini **Tanzania**, wanufaika wengi wamekuwa tegemezi wa ruzuku, karibia asilimia 60 ya wakulima wakipata kwa kurudia.
- ▶ Nchini **Zambia**, wakulima wadogo wamepoteza karibia 30% ya kipato chao pindi ruzuku zilivyoondolewa kwa muda mwaka 2013.
- ▶ Nchini **Zimbabwe**, utegemezi wa msaada wa moja kwa moja wa wakulima kwa serikali unailazimisha serikali kugeuka kuelekea kwenye mipango ya mikopo.

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo umewashawishi wakulima kuingia katika duru ya utegemezi wa pembejeo za Mapinduzi ya Kijani, ambazo zinaharibu rutuba ya udongo na kuathiri bioanuai ya kilimo, mfumo wa mbegu na maarifa ya wakulima na uhuru wao.

